ISSN 0856 - 034X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

**No. 8** **11th October, 2024**

***ACT SUPPLEMENT***

*To The Gazette of the United Republic of Tanzania No.42 Vol. 105 Dated 11th October, 2024*
Printed by The Government Printer, Dodoma by Order of Government

# SHERIA YA VIWANJA VYA NDEGE TANZANIA YA MWAKA 2024

## MPANGILIO WA VIFUNGU

*Kifungu* *Maelezo*

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina na tarehe ya kuanza kutumika.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI
MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE TANZANIA

4. Uanzishwaji wa Mamlaka.
5. Majukumu ya Mamlaka.
6. Madaraka ya Mamlaka.
7. Bodi ya Mamlaka.
8. Mamlaka ya Bodi.
9. Mkurugenzi Mkuu.
10. Watumishi wa Mamlaka.

SEHEMU YA TATU
USIMAMIZI, UENDESHAJI NA UENDELEZAJI WA VIWANJA VYA NDEGE VYA SERIKALI

*(a) Usimamizi wa Viwanja vya Ndege*

11. Tangazo la kiwanja cha ndege.
12. Rejesta ya taarifa za viwanja vya ndege.
13. Mkurugenzi na meneja wa kiwanja cha ndege.
14. Kamati za kiwanja cha ndege.

15. Utoaji wa huduma na uendeshaji wa biashara kwenye viwanja vya ndege.
16. Ada na tozo kwa huduma za viwanja vya ndege.
17. Eneo la ukomo wa vizuizi.

*(b) Uendeshaji wa Viwanja vya ndege*

18. Miongozo ya uendeshaji wa viwanja vya ndege.
19. Ubora wa huduma katika kiwanja cha ndege.
20. Ulinzi kwenye viwanja vya ndege.
21. Usalama katika kiwanja cha ndege.
22. Usimamizi wa maegesho ya ndege.
23. Ukamataji wa watumishi wa Mamlaka.
24. Uondoaji wa ndege, chombo cha usafiri na kifaa kilichoharibika.
25. Utunzaji na uhifadhi wa bidhaa hatarishi.
26. Dharura na matukio yasiyotarajiwa kwenye viwanja vya ndege.
27. Usimamizi wa mazingira.

*(c) Uendelezaji wa Viwanja vya ndege*

28. Uchaguzi wa maeneo, mipango, usanifu na ujenzi wa viwanja vya ndege.
29. Utunzaji wa viwanja vya ndege.
30. Usimamizi wa ardhi, miundombinu na mali kwenye viwanja vya ndege.
31. Ushauri wa uendeshaji wa viwanja binafsi vya ndege.

SEHEMU YA NNE
MASHARTI YA FEDHA

32. Vyanzo vya fedha za Mamlaka.
33. Matumizi ya fedha.
34. Bajeti ya Mamlaka.
35. Hesabu na ukaguzi.
36. Taarifa ya mwaka.
37. Uwekezaji na usimamizi wa mali.

SEHEMU YA TANO
MAKOSA NA ADHABU

38. Makosa.

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

39. Umiliki wa vitu hatari katika maeneo yaliyozuiliwa au yanayodhibitiwa.
40. Udanganyifu.
41. Adhabu ya jumla.
42. Kufifilisha makosa.

SEHEMU YA SITA
MASHARTI MENGINEYO

43. Mamlaka ya kutoa maelekezo.
44. Miongozo ya Mdhibiti.
45. Kinga dhidi ya uwajibikaji binafsi.
46. Kanuni.
47. Kufutwa kwa Sheria.

MAJEDWALI

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

**NA. 8 YA 2024**

NAKUBALI

SAMIA SULUHU HASSAN
*Rais*

[2 Oktoba, 2024]

**Sheria ya kuanzisha mamlaka ya viwanja vya ndege Tanzania, kuainisha majukumu na madaraka yake; kuweka masharti ya uanzishaji, uendelezaji, usimamizi, uendeshaji na utunzaji wa viwanja vya ndege na masuala mengine yanayohusiana na hayo.**

**IMETUNGWA** na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina na tarehe ya kuanza kutumika

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Viwanja vya Ndege Tanzania ya mwaka 2024 na itaanza kutumika tarehe ambayo Waziri atateua kwa notisi itakayochapishwa katika Gazeti la Serikali.

Matumizi

**2**. Sheria hii itatumika kwa masuala yote yanayohusu uendelezaji, usimamizi, uendeshaji na utunzaji wa viwanja vya ndege vilivyopo Tanzania Bara.

Tafsiri

**3**. Katika Sheria hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"bidhaa hatarishi" maana yake ni kitu au kemikali inayoweza kuhatarisha afya ya binadamu, mazingira au mali;

"Bodi" maana yake ni Bodi ya Mamlaka iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 7;

"eneo lililo karibu na kiwanja cha ndege" maana yake ni eneo la mzunguko lililo katika kipenyo cha maili tano za bahari kutoka katikati ya barabara ya kuruka na kutua ndege;

"eneo la mjongeo" maana yake ni sehemu za barabara za viungio zinazounganisha barabara za kuruka na kutua ndege na eneo la maegesho ya ndege katika kiwanja cha ndege;

"eneo la ukomo wa kizuizi" maana yake ni eneo ndani na karibu ya kiwanja cha ndege lisilopaswa kuwa na kizuizi ili kuruhusu shughuli za ndege zilizokusudiwa kufanyika kwa usalama;

"huduma za kiwanja cha ndege" maana yake ni huduma na vifaa vyote vinavyotolewa na Mamlaka katika viwanja vya ndege kwa ajili ya huduma za ndege, abiria, mizigo na barua;

"kamati za viwanja vya ndege" maana yake ni kamati zitakazoundwa kwa mujibu wa kifungu cha 14;

"kitu kilichokatazwa" maana yake ni kitu kinachoweza kutumika kutenda kitendo cha uvamizi;

"kitendo cha uvamizi" maana yake ni kitendo cha kuingia au kupanga kuingia mahali au eneo lisiloruhusiwa au kuingilia taratibu za utendaji kazi kinachoweza kuhatarisha ulinzi na usalama wa usafiri wa anga;

"kiwanja cha ndege" maana yake ni eneo lililotengwa juu ya ardhi au maji ambalo limekusudiwa kutumika lote au kwa sehemu kwa ajili ya ndege kutua, kuondoka, kuendeshwa na kuegeshwa zikiwa ardhini, na inajumuisha majengo, mitambo na vifaa vyovyote vilivyopo katika eneo hilo;

"kiwanja binafsi cha ndege" maana yake ni kiwanja cha ndege kinachomilikiwa, kuendelezwa au kusimamiwa na-

(a) mtu yeyote isipokuwa Mamlaka; au
(b) mtu yeyote pamoja na Mamlaka ambapo mtu huyo anamiliki zaidi ya asilimia hamsini ya hisa katika mali za kiwanja hicho cha ndege;

"kizuizi" maana yake ni kitu au sehemu ya kitu chochote -
(a) kilicho katika eneo lililokusudiwa kwa ajili ya kuendeshea ndege zikiwa ardhini;
(b) kinachovuka usawa wa eneo lililoainishwa kwa ajili ya kulinda ndege zinaporuka; au
(c) kilicho nje ya eneo lililoainishwa na baada ya tathmini kimeonekana kuwa ni hatari kwa usafiri wa anga;

"maegesho ya ndege" maana yake ni eneo lililotengwa katika kiwanja cha ndege ambalo limekusudiwa kutumika na ndege kwa madhumuni ya kupakia au kushusha abiria, mizigo au vifurushi, kuweka mafuta, maegesho au matengenezo;

"Mamlaka" maana yake ni Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 4;

Sura ya 80

"Mdhibiti" maana yake ni Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Usafiri wa Anga;

"miundombinu ya kiwanja cha ndege" maana yake ni mfumo wa kimuundo na vifaa vinavyohitajika kwa ufanisi wa shughuli zote zinazohusiana na kiwanja cha ndege na inajumuisha barabara za kuruka na kutua ndege, majengo na vifaa vingine vya kusaidia ndege wakati wa kutua, kuruka na wakati zinapokuwa ardhini;

"Mkurugenzi Mkuu" maana yake ni Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka anayeteuliwa chini ya kifungu cha 9;

"muendeshaji wa kiwanja binafsi cha ndege" maana yake ni mtu mwenye leseni au aliyesajiliwa kuendesha kiwanja binafsi cha ndege;

"ndege" maana yake ni chombo cha usafiri wa anga;

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Viwanja vya Ndege Tanzania;

"tozo zisizohusiana na shughuli za usafiri wa anga" maana

yake ni ada na tozo zisizohusiana moja kwa moja na huduma za usafiri wa anga;

"viwanja vya ndege vinavyomilikiwa na Serikali" maana yake ni viwanja vya ndege vilivyoainishwa katika Jedwali la Pili na viwanja vingine vyovyote vitakavyoanzishwa na Serikali kwa upande wa Tanzania Bara au kutamkwa kuwa viwanja vya ndege;

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya viwanja vya ndege.

## SEHEMU YA PILI
## MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE TANZANIA

Uanzishwaji wa Mamlaka

**4**.-(1) Inaanzishwa Mamlaka itakayojulikana kama Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania itakayojulikana pia kama "TAA".

(2) Mamlaka itakuwa ni chombo hodhi chenye urithishaji endelevu na lakiri yake, na kwa jina lake, itakuwa na uwezo wa-

(a) kushtaki na kushtakiwa;
(b) kupata, kumiliki na kuondosha mali;
(c) kukopa na kukopesha;
(d) kuingia kwenye mikataba au taratibu nyinginezo; na
(e) kutumia mamlaka na kutekeleza majukumu iliyopewa chini ya Sheria hii.

Majukumu ya Mamlaka

**5**. Mamlaka itakuwa na majukumu yafuatayo:

(a) kupanga, kuandaa na kutekeleza mipango kwa ajili ya ujenzi, uendelezaji, uendeshaji, usimamizi na utunzaji wa miundombinu, majengo na vifaa vya viwanja vya ndege vya Serikali;

(b) kutoa ushauri wa kitaalamu kwa Serikali na umma kuhusu masuala ya kitaifa na kimataifa kuhusu uanzishwaji, uendelezaji, usimamizi, uendeshaji na utunzaji wa viwanja vya ndege;
(c) kutoa vifaa muhimu vya viwanja vya ndege,

huduma za ulinzi na usalama na huduma nyingine zinazohusiana na hizo kwa ajili ya kuwezesha ndege, abiria, mizigo na vifurushi kwa viwanja vya ndege vya Serikali;

(d) kusimamia shughuli za kila siku za viwanja vya ndege vya Serikali kwa kuzingatia kanuni na viwango;

(e) kuhakikisha huduma za zimamoto na uokoaji zinatolewa katika viwanja vya ndege vya Serikali;

(f) kutunza ardhi za viwanja vya ndege na kufuatilia ujenzi na uwekaji wa vizuizi katika maeneo ya karibu na viwanja vya ndege vya Serikali;

(g) kusimamia utunzaji na uhifadhi wa bidhaa hatarishi ndani ya viwanja vya ndege vya Serikali;

(h) kushughulikia dharura zinazohusu masuala ya uendeshaji ndani ya viwanja vya ndege vya Serikali na maeneo ya jirani;

(i) kuvitangaza viwanja vya ndege vya Serikali, kuvutia mashirika ya ndege na kuibua fursa za kibiashara;

(j) kuweka na kutunza vifaa vya kisasa vya teknolojia ya habari na mawasiliano ili kuimarisha shughuli za viwanja vya ndege vya Serikali;

(k) kuanzisha taasisi za mafunzo kwa ajili ya mafunzo ya usimamizi wa viwanja vya ndege na karakana kwa ajili ya matengenezo ya vifaa na mitambo ya Mamlaka;

(l) kutoa huduma za ushauri elekezi kuhusu uendelezaji na usimamizi wa viwanja vya ndege ndani au nje ya nchi; na

(m) kutekeleza majukumu mengine ambayo yanaweza kutolewa kwa Mamlaka na Sheria hii au sheria nyingine yoyote.



PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

Madaraka ya Mamlaka

**6**. Katika utekelezaji wa majukumu yake chini ya Sheria hii, Mamlaka itakuwa na madaraka ya-

(a) kumtaka mtumiaji wa eneo karibu na kiwanja cha ndege kuondoa kitu chochote au kusitisha shughuli yoyote ambayo inaweza kuhatarisha shughuli za uendeshaji wa kiwanja cha ndege kwa kushirikiana;

(b) kuingia kwenye eneo au jengo lolote karibu na kiwanja cha ndege kwa madhumuni ya kuzuia kitu chochote kuingia kwenye eneo la ukomo wa vizuizi kwa kushirikiana;

(c) kuzuia ufikiaji wa sehemu yoyote ya kiwanja cha ndege kwa kuzingatia taratibu zote husika baada ya kupata vibali vinavyohitajika;

(d) kuingia katika makubaliano ya ukodishaji, uendeshaji, usimamizi, utoaji wa huduma au aina nyingine yoyote ya makubaliano na taasisi binafsi au ya Serikali kwa madhumuni ya kukasimu jukumu la Mamlaka kwa taasisi hiyo kutekeleza shughuli za Mamlaka kama itakavyoainishwa katika makubaliano husika;

(e) kuanzisha rejesta ya taarifa za viwanja vya ndege ya Serikali; na

(f) kupanga na kuainisha ada na tozo za huduma za viwanja vya ndege zisizohusiana na usafiri wa anga.

Bodi ya Mamlaka

**7**.-(1) Inaanzishwa Bodi ya Mamlaka ambayo itakuwa chombo cha usimamizi chenye jukumu la kusimamia shughuli na masuala yote ya Mamlaka.

(2) Bodi ya Mamlaka itakuwa na wajumbe wafuatao:

(a) Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais;

(b) wajumbe wengine sita ambao watateuliwa na Waziri kama ifuatavyo:

(i) mwakilishi kutoka Wizara yenye dhamana ya usafiri wa anga;

(ii) mwakilishi kutoka Wizara yenye

dhamana ya fedha;

(iii) Afisa Sheria anayemwakilisha Mwanasheria Mkuu wa Serikali;

(iv) mtu mwenye ujuzi na uzoefu katika masuala ya ujenzi wa viwanja vya ndege;

(v) mwakilishi kutoka miongoni mwa waendeshaji wa viwanja binafsi vya ndege; na

(vi) mtu mwenye ujuzi na uzoefu katika taaluma ya usafiri wa anga, utawala, uchumi, utalii, sheria, uhandisi au taaluma nyingine inayohusiana na hizo.

(3) Waziri atazingatia jinsia katika kuteua wajumbe wa Bodi katika kifungu kidogo cha (2)(b).

(4) Masuala kuhusu muda wa kushika wadhifa na taratibu nyingine za Bodi zitakuwa kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

(5) Mkurugenzi Mkuu atakuwa Katibu wa Bodi.

Mamlaka ya Bodi

**8**. Katika kusimamia shughuli za Mamlaka, Bodi itakuwa na mamlaka ya-

(a) kuidhinisha mipango, bajeti, taarifa za mwaka na hesabu za Mamlaka;

(b) kupitia muundo wa Mamlaka, mpango wa motisha, kanuni za watumishi na miongozo ya kiutawala na kupendekeza ziidhinishwe na mamlala husika;

(c) kupitisha kanuni za maadili kwa watumishi wa Mamlaka;

(d) kuidhinisha ada na tozo zisizohusiana na shughuli za usafiri wa anga; na

(e) kufanya masuala mengine ambayo ni muhimu au yanafaa katika kuhakikisha utendaji bora wa majukumu ya Mamlaka chini ya Sheria hii.

Mkurugenzi Mkuu

**9**.-(1) Kutakuwa na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ambaye atateuliwa na Rais.

(2) Mtu anaweza kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu ikiwa-

(a) ana angalau shahada ya uzamili kutoka chuo kikuu kinachotambulika; na

(b) ana uzoefu wa kufanya kazi kwa angalau miaka kumi katika nyanja ya usafiri wa anga, uchukuzi, uhandisi, sheria, usimamizi wa biashara, rasilimali watu au uchumi.

(3) Mkurugenzi Mkuu atashika wadhifa kwa kipindi cha miaka mitano na anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kingine kimoja.

(4) Mkurugenzi Mkuu atakuwa afisa mtendaji mkuu na afisa masuuli wa Mamlaka.

(5) Mkurugenzi Mkuu atakuwa na wajibu wa-

(a) kusimamia utekelezaji wa shughuli za kila siku za Mamlaka;

(b) kutekeleza maamuzi ya Bodi;

(c) kusimamia watumishi wa Mamlaka na watumishi wa taasisi nyingine wanaotekeleza majukumu yao katika viwanja vya ndege vya Serikali; na

(d) kutekeleza majukumu mengine kama atavyoelekezwa na Bodi.

Watumishi wa Mamlaka

**10**.-(1) Mamlaka inaweza kuajiri watumishi na wafanyakazi wengine katika kada na ngazi mbalimbali kadri itakavyoonekana ni muhimu kwa ajili ya utekelezaji bora wa majukumu ya Mamlaka.

(2) Mkurugenzi Mkuu atakuwa ni mamlaka ya nidhamu kwa watumishi na wafanyakazi wa Mamlaka.

## SEHEMU YA TATU
## USIMAMIZI, UENDESHAJI NA UENDELEZAJI WA VIWANJA VYA NDEGE VYA SERIKALI

### *(a) Usimamizi wa Viwanja vya Ndege*

Tangazo la kiwanja cha ndege

**11**.-(1) Viwanja vya ndege vilivyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria hii vitachukuliwa kuwa vimetangazwa kuwa viwanja vya ndege vya Serikali kwa



PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

madhumuni ya Sheria hii au sheria nyingine yoyote.

(2) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1), Waziri anaweza, kwa notisi itakayochapishwa kwenye Gazeti la Serikali, kurekebisha Jedwali la Pili.

Rejesta ya taarifa za viwanja vya ndege

**12**.-(1) Mamlaka itaanzisha na kutunza rejesta ya taarifa za viwanja vya ndege ambayo itakuwa na taarifa zifuatazo:

(a) viwanja vyote vya ndege vya Serikali vilivyopo Tanzania Bara;

(b) taarifa za uendeshaji wa kiwanja cha ndege zinazojumuisha maelezo kuhusu hali ya umiliki, mahali kiwanja cha ndege kilipo, ukubwa wa eneo la kiwanja husika, miundombinu, vifaa na mifumo, hali ya leseni, huduma zilizopo na matukio na ajali zilizotokea;

(c) takwimu za ndege kwenye kiwanja cha ndege ambazo ni pamoja na safari za ndege, idadi ya abiria, mizigo na vifurushi; na

(d) taarifa nyingine yoyote ambayo Mamlaka itaona ni muhimu.

(2) Kwa kuzingatia utaratibu utakaoainishwa, maelezo na taarifa zilizo katika rejesta ya taarifa za viwanja vya ndege zinaweza kutolewa kwa umma iwapo zitaombwa.

Mkurugenzi na meneja wa kiwanja cha ndege

**13**.-(1) Mkurugenzi Mkuu atateua mkurugenzi au meneja wa kiwanja cha ndege kwa ajili ya usimamizi wa viwanja vya ndege vya kimataifa au vya kitaifa.

(2) Mkurugenzi au meneja wa kiwanja cha ndege atakuwa na majukumu yafuatayo:

(a) kusimamia shughuli za kila siku za uendeshaji katika kiwanja cha ndege;

(b) kuhakikisha watu wanaotekeleza majukumu kwenye kiwanja cha ndege wanazingatia taratibu za ulinzi na usalama wa viwanja vya ndege; na

(c) kuhakikisha uzingatiaji wa masharti ya Sheria hii na sheria nyingine husika na viwango vya

kitaifa na kimataifa katika ngazi ya kiwanja.

Kamati za kiwanja cha ndege

**14**.-(1) Kutaanzishwa katika kila kiwanja cha ndege, kamati ya ulinzi, kamati ya usalama, kamati ya uwezeshaji au kamati nyingine yoyote inayohusiana na shughuli za uendeshaji wa kiwanja cha ndege.

(2) Muundo, kazi na taratibu za uendeshaji wa kamati zitakazoanzishwa chini ya kifungu hiki zitakuwa kama itakavyoainishwa katika nyaraka husika za uendeshaji.

(3) Kamati zitakazoanzishwa chini ya kifungu hiki zitakuwa na wajibu wa kuwasilishwa taarifa kwa Mamlaka kulingana na mwongozo wa uendeshaji wa kiwanja husika.

Utoaji wa huduma na uendeshaji wa biashara kwenye viwanja vya ndege

**15**.-(1) Mamlaka inaweza kuingia makubaliano na wapangaji na watoa huduma kwa ajili ya utoaji wa huduma mbalimbali kwenye viwanja vya ndege kwa vigezo na masharti kama yatakavyoainishwa katika mikataba husika.

(2) Katika kubainisha idadi ya watoa huduma wanaohitajika kwa huduma mbalimbali kwenye viwanja vya ndege, Mamlaka itazingatia vigezo vifuatavyo:

(a) ukubwa wa soko;
(b) miundombinu na vifaa vya kiwanja cha ndege vilivyopo;
(c) ulinzi na usalama wa kiwanja wa ndege;
(d) uwezo wa mtoa huduma katika kutoa huduma; na
(e) kigezo kingine chochote muhimu kama Mamlaka itakavyoamua.

Ada na tozo kwa huduma za viwanja vya ndege

**16**.-(1) Mamlaka, kwa notisi itakayochapishwa kwenye Gazeti la Serikali, itaainisha ada na tozo kwa huduma za viwanja vya ndege zisizohusiana na usafiri wa anga.

(2) Katika kuamua ada na tozo chini ya kifungu kidogo cha (1), Mamlaka itazingatia masuala yafuatayo:

(a) gharama ya kutoa huduma husika;
(b) gharama za utoaji huduma kama hizo kwa kulinganisha na viwanja vingine kikanda na kimataifa; na

(c) jambo lingine lolote ambalo Mamlaka itaona ni muhimu.

Eneo la ukomo wa vizuizi

**17**.-(1) Mtu hatajenga, hataruhusu kujengwa au kukua kwa kizuizi katika au karibu na kiwanja cha ndege ambacho kinahatarisha au kuzuia usalama wa ndege na uendeshaji wa shughuli za kiwanja cha ndege.

(2) Mamlaka itaainisha na kufuatilia eneo la ukomo wa vizuizi ndani ya maeneo ya karibu na viwanja vyake vya ndege ili kuhakikisha kuwa maeneo hayo hayazuiliwi na vitu, majengo au maendelezo mengine.

(3) Kwa madhumuni ya kufuatilia maeneo ya ukomo wa vizuizi katika viwanja vya ndege, Mamlaka inaweza kufanya ufuatiliaji na ukaguzi kwenye majengo yaliyo jirani na kiwanja cha ndege.

(4) Endapo kuna kizuizi kinachoingia eneo la ukomo wa kiwanja cha ndege, Mamlaka itamtaka mtu ambaye ameweka kizuizi hicho kukiondoa ndani ya muda utakaoainishwa.

(5) Endapo mtu atashindwa kuondoa kizuizi ndani ya muda ulioainishwa katika kifungu kidogo cha (4), Mamlaka itaondoa kizuizi hicho kwa gharama za mtu huyo.

*(b) Uendeshaji wa Viwanja vya Ndege*

Miongozo ya uendeshaji wa viwanja vya ndege

**18**.-(1) Mamlaka itaendesha shughuli za viwanja vya ndege kwa mujibu wa miongozo ya uendeshaji wa viwanja vya ndege iliyoidhinishwa na Mdhibiti.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1), Mamlaka inaweza kuandaa taratibu na miongozo inayoainisha-

(a) udhibiti wa watu, vyombo vya usafiri na vifaa kwenye maeneo ya viwanja vya ndege;
(b) udhibiti wa mijongeo ya ndege kwenye eneo la maegesho ya ndege;
(c) mazoezi ya utayari wa kukabiliana na dharura;
(d) hatua za ulinzi dhidi ya vitendo vya uvamizi;
(e) ulinzi na usimamizi wa mali na vifaa vya

viwanja vya ndege;
(f) udhibiti wa hatari ya wanyama na ndege hai kwenye shughuli za uendeshaji wa viwanja vya ndege;
(g) usimamizi wa mazingira;
(h) uondoaji wa ndege, chombo cha usafiri au kifaa kilichoharibika;
(i) utunzaji na uhifadhi wa bidhaa hatarishi; na
(j) suala lingine lolote linalohusiana na uendeshaji wa viwanja vya ndege.

(3) Mamlaka itahuisha miongozo na taratibu za uendeshaji kadri inavyotakiwa na Mdhibiti.

Ubora wa huduma katika kiwanja cha ndege

**19**. Mamlaka itaweka utaratibu wa uendeshaji wa kiwanja cha ndege utakaoepusha ucheleweshaji wa ndege, abiria, mizigo na vifurushi katika viwanja vya ndege kwa-
(a) kuhakikisha ndege inayowasili au kuondoka inahudumiwa kwa mujibu wa viwango vya huduma vitakavyoainishwa katika miongozo ya uendeshaji wa kiwanja cha ndege cha Serikali;
(b) kuweka miundombinu, vifaa, mifumo, na kutoa huduma nyingine za viwanja vya ndege zinazohusika; na
(c) kuwezesha upatikanaji wa huduma muhimu zinazotolewa na taasisi nyingine za Serikali.

Ulinzi kwenye viwanja vya ndege

**20**. Mamlaka itahakikisha kuwa-
(a) mpango wa ulinzi wa kila kiwanja cha ndege unaandaliwa na kutekelezwa;
(b) ufuatiliaji, doria na ulinzi unafanywa ili kuhakikisha usalama katika maeneo yanayodhibitiwa na kuzuiliwa katika kiwanja cha ndege na maeneo ya jirani;
(c) uingiaji kwenye maeneo ya viwanja vya ndege unadhibitiwa;
(d) vitu visivyoruhusiwa haviingizwi ndani ya ndege;
(e) huduma za ulinzi katika kiwanja cha ndege zinatolewa na watu wenye mafunzo stahiki; na
(f) kiwanja cha ndege kina mifumo na vifaa vya



PARLIAMENT OF TANZANIA BUNGE LA TANZANIA

kisasa vya ulinzi.

Usalama katika kiwanja cha ndege

**21**. Mamlaka itahakikisha kuwa-

(a) huduma za zimamoto na uokoaji zinatolewa katika viwanja vya ndege;

(b) mpango wa udhibiti wa hatari ya wanyama na ndege hai kwenye shughuli za uendeshaji wa viwanja vya ndege umeandaliwa na kutekelezwa; na

(c) mfumo wa usimamizi wa usalama kwenye viwanja vya ndege umeandaliwa na kutekelezwa.

Usimamizi wa maegesho ya ndege

**22**. Mamlaka itaandaa na kutekeleza mpango wa usimamizi wa maegesho ya ndege.

Ukamataji wa watumishi wa Mamlaka

**23**.-(1) Endapo uendeshaji salama wa kiwanja cha ndege au huduma nyingine saidizi unaweza kuhatarishwa kutokana na kukamatwa kwa mtumishi yeyote, kwa hati ya ukamataji au bila hati, afisa wa polisi anayetekeleza jukumu la ukamataji atamjulisha kwanza mkurugenzi au meneja wa kiwanja cha ndege husika na kisha kumkamata mtumishi huyo.

(2) Kwa madhumuni ya kuhakikisha uendeshaji salama wa kiwanja cha ndege, mkurugenzi au meneja atateua mtumishi mwingine wa kutekeleza majukumu ya mtumishi aliyekamatwa.

Uondoaji wa ndege, chombo cha usafiri na kifaa kilichoharibika

**24**.-(1) Mwendeshaji wa ndege, chombo cha usafiri au kifaa kilichoharibika atawajibika kuondoa ndege, chombo cha usafiri au kifaa hicho katika eneo la mjongeo wa ndege kwa kuzingatia mwongozo wa uondoaji wa ndege, vyombo vya usafiri au vifaa vilivyoharibika.

(2) Endapo mwendeshaji atashindwa kuondoa mara moja ndege, chombo cha usafiri au kifaa kilichoharibika, Mamlaka itaondoa ndege, chombo cha usafiri au kifaa hicho kutoka eneo la mjongeo wa ndege kwa gharama ya mwendeshaji.

(3) Mamlaka au mwendeshaji hataondoa ndege

ambayo imehusika katika ajali isipokuwa kama taratibu husika zilizowekwa na Mdhibiti zimezingatiwa.

Utunzaji na uhifadhi wa bidhaa hatarishi

**25**.-(1) Mamlaka inaweza kuruhusu utunzaji na uhifadhi wa bidhaa hatarishi kwenye viwanja vya ndege iwapo mmiliki wa bidhaa husika ana kibali halali kutoka kwa Mdhibiti kwa ajili ya usafirishaji na uhifadhi wa bidhaa hizo.

(2) Katika kushughulikia bidhaa hatarishi, Mamlaka itahakikisha upatikanaji wa vifaa vya utunzaji na uhifadhi wa bidhaa hatarishi na uwepo wa watumishi wenye mafunzo stahiki.

(3) Utaratibu wa kutunza na kuhifadhi bidhaa hatarishi katika viwanja vya ndege utazingatia miongozo itakayotolewa na Mdhibiti.

Dharura na matukio yasiyotarajiwa kwenye viwanja vya ndege

**26**. Mamlaka, kwa kuzingatia miongozo itakayotolewa na Mdhibiti, itaandaa na kutekeleza mipango ya kukabiliana na dharura na matukio yasiyotarajiwa kwenye viwanja vya ndege inayoendana na shughuli za uendeshaji na shughuli nyingine katika kiwanja cha ndege.

Usimamizi wa mazingira

**27**.-(1) Mamlaka itaandaa mpango wa usimamizi wa mazingira wa kiwanja cha ndege na kuhakikisha utekelezaji wa mpango huo unapunguza athari ya hatari au hatari tarajiwa.

(2) Katika utekelezaji wa wajibu chini ya kifungu hiki, Mamlaka itazingatia viwango na kanuni za mazingira za kitaifa na kimataifa.

*(c) Uendelezaji wa Viwanja vya Ndege*

Uchaguzi wa maeneo, mipango, usanifu na ujenzi wa viwanja vya ndege

**28**.-(1) Mamlaka inaweza kuanzisha kiwanja cha ndege katika sehemu yoyote ya Tanzania Bara iwapo uanzishwaji huo ni muhimu kwa kuzingatia mahitaji ya usafiri wa anga, faida za kiuchumi na kijamii au maslahi ya umma kwa kuzingatia miongozo itakayotolewa na Mdhibiti.

(2) Katika kuanzisha kiwanja cha ndege kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1), Mamlaka-



PARLIAMENT OF TANZANIA BUNGE LA TANZANIA

(a) itafanya uchaguzi wa eneo la kiwanja cha ndege;
(b) itaanda mipango ya uboreshaji wa viwanja vya ndege vilivyopo au ujenzi wa viwanja vya ndege vipya na kuhakikisha mipango hiyo inaweza kukidhi upanuzi wowote wa siku zijazo; na
(c) itasanifu, itajenga, itakarabati na kufanya upanuzi wa miundombinu na vifaa vya kiwanja cha ndege ikiwemo mitambo yoyote husika.

Utunzaji wa viwanja vya ndege

**29**.-(1) Mamlaka itatunza viwanja vya ndege vilivyo chini yake kwa kuanzisha na kutekeleza mpango wa ukarabati ili kuhakikisha kuwa vifaa viko katika hali ya ubora inayoruhusu uendeshaji bora wa viwanja vya ndege.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1), vifaa vitajumuisha miundombinu, mifumo na mitambo ya viwanja vya ndege, majengo na vifaa vingine vinavyofanana na hivyo.

Usimamizi wa ardhi, miundombinu na mali kwenye viwanja vya ndege

**30**.-(1) Mamlaka itakuwa msimamizi wa ardhi iliyotengwa kwa ajili ya kiwanja cha ndege cha Serikali, ikijumuisha mali, miundombinu, mifumo na majengo yote, na itakuwa na mamlaka ya-
(a) kupanga matumizi;
(b) kuzuia watu au viumbe hai kuingia kwenye ardhi ya kiwanja cha ndege; na
(c) kuidhinisha uwekaji wa miundombinu, vifaa na mifumo kwenye kiwanja cha ndege.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1), Mamlaka inaweza kutoa amri au maelekezo na kuchukua hatua stahiki kwa ajili ya kuhakikisha usimamizi bora wa kiwanja cha ndege.

(3) Amri au maelekezo ya Mamlaka katika kifungu hiki yanaweza kujumuisha matengenezo ya vifaa, malipo ya ada au tozo, uendeshaji wa shughuli za biashara na masuala mengine ya usimamizi wa kiwanja cha ndege.

Ushauri wa uendeshaji wa

**31**.-(1) Mamlaka inaweza kushauri kuhusu uendeshaji wa viwanja binafsi vya ndege vya Tanzania

viwanja binafsi vya ndege

Bara.

(2) Kwa madhumuni ya kutekeleza jukumu lake chini ya kifungu kidogo cha (1), Mamlaka inaweza-

(a) kutoa ushauri au msaada wa kitaalamu katika uanzishwaji wa viwanja binafsi vya ndege;

(b) kumshauri Mdhibiti kuhusu masuala yanayohusiana na uendeshaji, ulinzi na usalama wa viwanja binafsi vya ndege.

## SEHEMU YA NNE
## MASHARTI YA FEDHA

Vyanzo vya fedha za Mamlaka

**32**. Vyanzo vya fedha vya Mamlaka vitajumuisha-

(a) kiasi cha fedha ambacho kitatengwa na Bunge;

Sura ya 365

(b) tozo ya huduma kwa abiria inayotozwa kwa mujibu wa Sheria ya Tozo ya Huduma za Viwanja vya Ndege;

(c) ada na tozo mbalimbali;

(d) fedha zitakazopatikana kwa njia ya msaada, gawio, zawadi au michango yoyote itakayotolewa kwa Mamlaka; na

(e) fedha nyingine yoyote inayoweza kupatikana au kupokelewa na Mamlaka katika utekelezaji wa majukumu na shughuli zake chini ya Sheria hii.

Matumizi ya fedha

**33**. Fedha za Mamlaka kwa mwaka wowote wa fedha zitatumika katika kulipia gharama zifuatazo:

(a) gharama za uendeshaji wa shughuli za Mamlaka;

(b) matumizi ya uendelezaji na utunzaji wa miundombinu, majengo, vifaa, mifumo na mitambo; na

(c) matumizi mengine yoyote yatakayoidhinishwa na Bodi.

Bajeti ya Mamlaka

**34**.-(1) Mkurugenzi Mkuu atatayarisha na kuwasilisha kwa Bodi bajeti ya mwaka wa fedha unaofuata kwa ajili ya kuidhinishwa kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Bajeti.

Sura ya 439

(2) Wakati wowote kabla ya mwisho wa mwaka wa

fedha, Mkurugenzi Mkuu anaweza kuandaa na kuwasilisha kwa Bodi makadirio yoyote ya nyongeza ya bajeti ya mwaka wa fedha husika kwa ajili ya kuidhinishwa.

(3) Matumizi hayatafanyika kwa fedha za Mamlaka isipokuwa kama yameidhinishwa na Bodi katika makadirio ya mwaka wa fedha husika au katika nyongeza ya bajeti ya mwaka husika.

(4) Bajeti ya mwaka au bajeti yoyote ya nyongeza iliyoidhinishwa na Bodi itawasilishwa kwa Waziri kwa ajili ya kuidhinishwa.

(5) Waziri anaweza kuitaka Mamlaka kufanya marekebisho ya bajeti ikiwa kwa maoni yake bajeti hiyo haiakisi makadirio sahihi na yenye uhalisia wa mapato na matumizi ya Mamlaka.

Hesabu na ukaguzi

**35**.-(1) Mamlaka itatunza na kuhifadhi vitabu vya hesabu na kumbukumbu nyingine zinazohusiana na shughuli zake na kuandaa taarifa ya hesabu ya mwaka kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Umma.

Sura ya 348

(2) Hesabu za Mamlaka zitakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali au afisa aliyeidhinishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Sura ya 418

(3) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Mamlaka itawasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hesabu za Mamlaka zikiwa zimeambatishwa na-

(a) taarifa ya utendaji wa kifedha katika mwaka husika;

(b) taarifa ya hali ya kifedha ya Mamlaka katika siku ya mwisho ya mwaka husika; na

(c) taarifa au hesabu nyingine kama itakavyohitajika ili kubainisha kwa ukamilifu mali, madeni, faida, hasara na shughuli za Mamlaka.

(4) Hesabu za Mamlaka kama ambavyo zitakuwa zimethibitishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali au mtu mwingine yeyote aliyeteuliwa kwa niaba yake pamoja na taarifa ya ukaguzi zitawasilishwa kwa Waziri kila mwaka.

(5) Waziri atawasilisha Bungeni hesabu na taarifa ya ukaguzi iliyopokelewa chini ya kifungu kidogo cha (4) ndani ya miezi mitatu baada ya kupokea taarifa hiyo au katika kikao cha Bunge kinachofuata, chochote kitakachotangulia kati ya hivyo.

Taarifa ya mwaka

**36**.-(1) Mamlaka itaandaa taarifa ya mwaka kuhusiana na mwaka wa fedha uliopita na kuwasilisha taarifa hiyo kwa Waziri ambaye ataiwasilisha Bungeni.

(2) Taarifa ya mwaka itajumuisha-

(a) maelezo ya kina kuhusu utendaji wa Mamlaka kwa mwaka husika;

(b) nakala ya hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka pamoja na taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali; na

(c) taarifa nyingine yoyote ambayo Mamlaka itahitajika kutoa chini ya Sheria hii.

Uwekezaji na usimamizi wa mali

**37**. Mamlaka inaweza kuwekeza sehemu yoyote ya fedha zake katika uwekezaji utakaoidhinishwa na Bodi na kuridhiwa na Waziri.

SEHEMU YA TANO
MAKOSA NA ADHABU

Makosa

**38**. Mtu ambaye-

(a) bila idhini au ikiwa siyo mtumishi wa Mamlaka au abiria-

(i) anapatikana katika eneo lolote lililozuiliwa au linalodhibitiwa au eneo lililotengwa na Mamlaka kama eneo hatari;

(ii) anakataa kuondoka katika eneo la kiwanja cha ndege au katika chombo cha usafiri kilicho katika kiwanja cha ndege, baada ya kuamriwa kuondoka na mtumishi wa Mamlaka au afisa wa polisi;

(b) akiwa katika eneo lolote la kiwanja cha ndege-

(i) anatenda kitendo chochote au anafanya



PARLIAMENT OF TANZANIA BUNGE LA TANZANIA

kitu chochote kinachoweza kusababisha madhara kwa mtu yeyote kwenye eneo hilo au chombo cha usafiri;

(ii) bila sababu ya msingi anakiuka maelekezo yoyote halali yaliyotolewa na mtumishi wa Mamlaka au afisa wa polisi;

(iii) anavuta sigara katika chombo cha usafiri au katika sehemu yoyote ya eneo la kiwanja cha ndege ambapo uvutaji wa sigara hauruhusiwi;

(c) anaondoa, anaharibu au anaingilia kinyume cha sheria mali yoyote ya Mamlaka iliyo katika eneo la kiwanja cha ndege;

(d) anazuia au kuingilia matumizi sahihi ya kiwanja cha ndege;

(e) anatupa au anaacha kitu chochote kinachoweza kusababisha madhara kwa mtu yeyote au uharibifu wa mali au miundombinu yoyote;

(f) bila sababu halali anafanya kitendo chochote kinachozuia au kinachoweza kuzuia magari kuondoka kwa uhuru katika kiwanja cha ndege au matumizi ya barabara, eneo la maegesho au miundombinu inayohusika;

(g) anashindwa kuwasilisha kwa mtumishi wa Mamlaka mali yoyote ambayo kuna sababu ya kuamini kuwa imepotea, imesahaulika au kupatikana kwenye eneo lolote la kiwanja cha ndege;

(h) kwa makusudi anamzuia mtumishi wa Mamlaka katika utekelezaji wa majukumu yake chini ya Sheria hii; au

(i) bila idhini anaruhusu mnyama yoyote kuingia ndani ya kiwanja cha ndege,

anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni moja na isiyozidi shilingi milioni tano au kifungo kisichopungua miezi sita na kisichozidi miaka miwili au vyote.

Umiliki wa vitu hatari katika maeneo yaliyozuiliwa au yanayodhibitiwa

**39**. Mtu ambaye, bila idhini, anamiliki-

(a) bunduki au kitu chochote chenye mwonekano wa bunduki, kinachoweza au kisichoweza kufyatuliwa;

(b) kilipuzi au kitu chochote kilichotengenezwa au kubadilishwa ili kuwa na mwonekano wa kilipuzi, kinachoweza au kisichoweza kutoa mlipuko;

(c) kitu chochote kilichowekwa alama ili kuashiria kuwa ni kilipuzi au kina kilipuzi; au

(d) kitu chochote ambacho hakipo miongoni mwa aya (a) au (b) na ambacho kimetengenezwa au kubadilishwa ili kutumika kusababisha majeraha au kumlemaza mtu, au kuharibu mali,

katika eneo lililozuiliwa au linalodhibitiwa, anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni kumi na isiyozidi shilingi milioni hamsini au kifungo kisichopungua miaka miwili na kisichozidi miaka mitano au vyote.

Udanganyifu

**40**. Mtu yeyote ambaye, kwa kujua au kwa uzembe, anatoa maelezo ya uongo katika taarifa, madai au nyaraka nyingine yoyote inayohitajika na Mamlaka au iliyoidhinishwa na kuandaliwa kwa madhumuni ya Mamlaka chini ya Sheria hii, anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi laki tano na isiyozidi shilingi milioni tatu au kifungo kisichopungua miezi mitatu na kisichozidi miezi sita au vyote.

Adhabu ya jumla

**41**. Mtu yeyote ambaye anatenda kosa chini ya Sheria hii au kanuni zilizotengenezwa chini ya Sheria hii ambapo hakuna adhabu mahsusi iliyobainishwa, akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi laki tano na isiyozidi shilingi milioni tano au kifungo kisichopungua miezi sita na kisichozidi miaka miwili au vyote.

Kufifilisha makosa

**42**.-(1) Bila ya kujali masharti ya Sheria hii yanayohusiana na adhabu, endapo mtu anakiri kwa

maandishi kwamba ametenda kosa chini ya Sheria hii, Mkurugenzi Mkuu au mtu aliyeidhinishwa na Mkurugenzi Mkuu kwa maandishi anaweza, wakati wowote kabla ya kufunguliwa kwa mashtaka mahakamani, kufifilisha kosa hilo na kumuamuru mtu huyo kulipa kiasi cha fedha kisichozidi nusu ya kiasi cha faini ambayo mtu huyo angewajibika kulipa iwapo angetiwa hatiani kwa kosa hilo.

(2) Endapo mtu atashindwa kuzingatia amri ya ufifilishaji iliyotolewa chini ya kifungu hiki ndani ya muda ulioainishwa, Mkurugenzi Mkuu au mtu aliyeidhinishwa anaweza, pamoja na kiasi kilichoamriwa, kumtaka mtu huyo kulipa riba kwa kiwango kitakachoainishwa katika kanuni.

(3) Endapo mtu atashindwa kuzingatia kifungu kidogo cha (2), Mkurugenzi Mkuu anaweza kutekeleza amri ya ufifilishaji na riba inayopaswa kulipwa kwa namna sawa na amri ya mahakama.

(4) Fedha zote zitakazotozwa chini ya kifungu hiki zitalipwa kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali.

(5) Endapo kosa limefifilishwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) na shauri limefunguliwa dhidi ya mkosaji kwa kosa hilo, itakuwa ni utetezi kwa mkosaji kuthibitisha kwa kiwango cha kuiridhisha mahakama kwamba kosa analoshtakiwa nalo limefifilishwa chini ya kifungu kidogo cha (1).

(6) Mkurugenzi Mkuu atawasilisha kwa Mkurugenzi wa Mashtaka taarifa za kila robo mwaka za makosa yote yaliyofifilishwa chini ya kifungu hiki.

(7) Fomu na namna ya kufifilisha makosa itakuwa kama itakavyoainishwa katika kanuni zitakazotengenezwa chini ya Sheria hii.

## SEHEMU YA SITA
## MASHARTI YA JUMLA

Mamlaka ya kutoa maelekezo

**43**. Waziri anaweza kutoa kwa Mamlaka maelekezo mahsusi au ya jumla ya masuala ya kisera kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka na Mamlaka

itakuwa na wajibu wa kuzingatia maelekezo hayo.

Miongozo ya Mdhibiti

**44**. Katika kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria hii, Mamlaka itazingatia miongozo itakayotolewa na Mdhibiti.

Kinga dhidi ya uwajibikaji binafsi

**45**. Mtumishi wa Mamlaka au mjumbe wa Bodi hatafunguliwa mashtaka, madai au kuwajibishwa kwa kitendo au jambo lolote ikiwa kitendo au jambo husika lilitendwa au kutotendwa kwa nia njema katika utekelezaji wa majukumu yake kama mtumishi wa Mamlaka au mjumbe wa Bodi.

Kanuni

**46**.-(1) Waziri anaweza kutengeneza kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii.

(2) Bila ya kuathiri kifungu kidogo cha (1), Waziri anaweza kutengeneza kanuni zitakazoainisha-

(a) ada na tozo zisizohusiana na usafiri wa anga;
(b) namna ya kuwasilisha maombi au taarifa zinazohitajika chini ya Sheria hii;
(c) usimamizi, uendeshaji na uendelezaji wa viwanja vya ndege vya Serikali;
(d) utaratibu wa ufifilishaji wa makosa; na
(e) suala lolote ambalo linaweza kuainishwa kwa mujibu wa kifungu chochote cha Sheria hii kwa ajili ya usimamizi, uendeshaji na uendelezaji wa viwanja vya ndege.

Kufutwa kwa Sheria
Sheria Na. 1 ya 1974

**47**. Sheria ya Utoaji wa Leseni na Udhibiti wa Viwanja vya Ndege inafutwa.

______

**JEDWALI LA KWANZA**

______

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 7(4))*

TARATIBU ZA BODI

Muda wa

**1**.-(1) Mjumbe wa Bodi, isipokuwa kama uteuzi wake

kushika wadhifa

utatenguliwa au ataacha kuwa mjumbe kwa namna nyingine yoyote, atashika wadhifa kwa muda wa miaka mitatu na anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kingine kimoja.

(2) Bila kujali aya ndogo ya (1), mjumbe wa Bodi anaweza kujiuzulu wakati wowote kwa kutoa notisi kwa maandishi kwa mamlaka ya uteuzi.

Vikao vya Bodi

**2**.-(1) Bodi itakutana kwa kawaida angalau mara nne kwa mwaka kwa ajili ya kuendesha shughuli zake.

(2) Mwenyekiti anaweza kuitisha kikao cha Bodi cha dharura wakati wowote pale ambapo kuna jambo la dharura linalohitaji kuamuliwa na Bodi au pale ambapo kuna maombi ya wajumbe wasiopungua wanne.

(3) Mwenyekiti ataongoza kila kikao cha Bodi.

(4) Endapo katika kikao chochote cha Bodi Mwenyekiti hayupo, wajumbe waliohudhuria watamchagua mjumbe mmoja kati yao kuongoza kikao hicho.

(5) Bodi inaweza kumwalika mtu yeyote ambaye si mjumbe kuhudhuria na kushiriki katika majadiliano katika kikao chochote cha Bodi isipokuwa mtu huyo hatakuwa na haki ya kupiga kura.

Mgongano wa maslahi

**3**.-(1) Mjumbe wa Bodi atachukuliwa kuwa na mgongano wa maslahi ikiwa anapata maslahi ya kifedha au maslahi mengine yoyote kwa madhumuni ambayo yanakinzana na utendaji bora wa majukumu au mamlaka yake kama mjumbe wa Bodi.

(2) Endapo mjumbe wa Bodi ana mgongano wa maslahi kuhusiana na-

(a) jambo lolote lililo mbele ya Mamlaka kwa ajili ya kujadiliwa au kuamuliwa; au

(b) jambo lolote ambalo Mamlaka ingelitarajia kuja mbele yake kwa ajili ya kujadiliwa au kuamuliwa,

mjumbe huyo ataweka wazi maslahi aliyonayo na kujiepusha kushiriki au kuendelea kushiriki katika majadiliano au uamuzi wa jambo husika.

Akidi

**4**. Akidi katika kikao chochote cha Bodi itakuwa angalau wajumbe wanne.

Uamuzi wa Bodi

**5**.-(1) Kwa kuzingatia aya ndogo ya (2), masuala yanayopendekezwa kwenye kikao cha Bodi yataamuliwa kwa wingi wa kura za wajumbe waliohudhuria na kupiga kura, na endapo kura zitalingana, Mwenyekiti au mjumbe anayeongoza kikao atakuwa na kura ya nyongeza zaidi ya kura yake ya uamuzi.

(2) Bodi inaweza kufanya uamuzi bila kikao kwa kusambaza miongoni mwa wajumbe nyaraka zinazohusika na mawasilisho ya wajumbe kwa maandishi yatakuwa uamuzi wa Bodi, isipokuwa mjumbe yeyote anaweza kuomba uamuzi husika uahirishwe na suala hilo lijadiliwe katika kikao cha Bodi kitakachofuata.

Kamati

**6.**-(1) Bodi inaweza kuunda na kuteua kamati kutoka miongoni mwa wajumbe wake kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Bodi chini ya Sheria hii.

(2) Kamati ya Bodi inaweza kumwalika mtu yeyote kuhudhuria na kujadili suala mahsusi kama kamati itakavyoamua, isipokuwa mtu huyo hatakuwa na haki ya kupiga kura.

(3) Kamati ya Bodi itatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia maelekezo ya Bodi.

Ukasimishaji wa majukumu na mamlaka ya Bodi

**7.**-(1) Bodi inaweza kukasimu kwa kamati yake yoyote au kwa Mkurugenzi Mkuu majukumu au mamlaka yoyote iliyopewa na Sheria hii au sheria nyingine yoyote, isipokuwa mamlaka ya-

(a) kuidhinisha ada na tozo;
(b) kuidhinisha bajeti, taarifa za mwaka na hesabu za Mamlaka; na
(c) kupitisha kanuni za maadili.

(2) Majukumu au mamlaka yaliyokasimiwa yatatekelezwa na kamati ya Bodi au Mkurugenzi Mkuu kwa jina na kwa niaba ya Bodi.

Muhtasari wa vikao

**8**. Muhtasari wa kila kikao cha Bodi utaandikwa katika utaratibu sahihi na utaridhiwa au utasahihishwa na kuridhiwa na Bodi katika kikao cha Bodi kinachofuata na kusainiwa na Mwenyekiti au mjumbe aliyeongoza kikao kinachohusika na muhtasari huo pamoja na Katibu.

Kasoro kutobatilisha mwenendo wa Bodi

**9**. Kitendo chochote au mwenendo wa Bodi hautabatilishwa kutokana na nafasi ya mjumbe yeyote kuwa wazi au kasoro yoyote katika uteuzi wa mjumbe.

Ada na posho

**10**. Wajumbe wa Bodi watalipwa ada na posho kama zitakavyoidhinishwa na mamlaka husika.

Bodi kuweka taratibu za kujiendesha

**11**. Kwa kuzingatia masharti ya Jedwali hili, Bodi itajiwekea utaratibu wa kujiendesha.



PARLIAMENT OF TANZANIA BUNGE LA TANZANIA

---

**JEDWALI LA PILI**

---

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 11(1))*

VIWANJA VYA NDEGE VINAVYOMILIKIWA NA SERIKALI

| NA. | KIWANJA CHA NDEGE | WILAYA | MKOA |
|---|---|---|---|
| 1. | Arusha | Arusha | Arusha |
| 2. | Bukoba | Bukoba | Kagera |
| 3. | Dodoma | Dodoma | Dodoma |
| 4. | Geita | Chato | Geita |
| 5. | Ifakara | Kilombero | Morogoro |
| 6. | Inyonga | Mlele | Katavi |
| 7. | Iringa | Iringa | Iringa |
| 8. | Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Mwalimu Julius Nyerere | Ilala | Dar es Salaam |
| 9. | Kahama | Kahama | Shinyanga |
| 10. | Kasulu | Kasulu | Kigoma |
| 11. | Kibondo | Kibondo | Kigoma |
| 12. | Kigoma | Kigoma | Kigoma |
| 13. | Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro | Hai | Kilimanjaro |
| 14. | Kilosa | Kilosa | Morogoro |
| 15. | Kilwa Masoko | Kilwa Masoko | Lindi |
| 16. | Kirondatal | Iramba | Singida |
| 17. | Kondoa | Kondoa | Dodoma |
| 18. | Kongwa | Kongwa | Dodoma |
| 19. | Lake Manyara | Karatu | Arusha |
| 20. | Lindi | Lindi | Lindi |
| 21. | Liuli | Nyasa | Ruvuma |
| 22. | Loliondo | Ngorongoro | Arusha |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 23. | Mafia | Mafia | Pwani |
| 24. | Mafinga | Mafinga | Iringa |
| 25. | Manyoni | Manyoni | Singida |
| 26. | Masasi | Masasi | Mtwara |
| 27. | Mbamba Bay | Nyasa | Ruvuma |
| 28. | Mbeya | Mbeya | Mbeya |
| 29. | Mombo | Korogwe | Tanga |
| 30. | Morogoro | Morogoro | Morogoro |
| 31. | Moshi | Moshi | Kilimanjaro |
| 32. | Mpanda | Mpanda | Katavi |
| 33. | Mpwapwa | Mpwapwa | Dodoma |
| 34. | Mtwara | Mtwara | Mtwara |
| 35. | Mufindi | Mufindi | Iringa |
| 36. | Musoma | Musoma | Mara |
| 37. | Mvumi | Chamwino | Dodoma |
| 38. | Mwanza | Ilemela | Mwanza |
| 39. | Nachingwea | Nachingwea | Lindi |
| 40. | Newala | Newala | Mtwara |
| 41. | Ngara | Ngara | Kagera |
| 42. | Ngarenairobi | Siha | Kilimanjaro |
| 43. | Njombe | Njombe | Njombe |
| 44. | Nzega | Nzega | Tabora |
| 45. | Same | Same | Kilimanjaro |
| 46. | Shinyanga | Shinyanga | Shinyanga |
| 47. | Singida | Singida | Singida |
| 48. | Songea | Songea | Ruvuma |
| 49. | Songwe | Mbeya | Mbeya |
| 50. | Sumbawanga | Sumbawanga | Rukwa |
| 51. | Tabora | Tabora | Tabora |
| 52. | Tanga | Tanga | Tanga |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 53. | Tunduru | Tunduru | Ruvuma |
| 54. | Ukerewe | Ukerewe | Mwanza |
| 55. | Urambo | Urambo | Tabora |
| 56. | Utete | Rufiji | Pwani |
| 57. | Uvinza | Uvinza | Kigoma |
| 58. | Chunya | Chunya | Mbeya |
| 59. | Biharamulo | Biharamulo | Kagera |
| 60. | West Kilimanjaro | Siha | Kilimanjaro |
| 61. | Liwale | Liwale | Lindi |

Imetungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 28 Agosti, 2024.

NENELWA JOYCE MWIHAMBI
*Katibu wa Bunge*

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA